**HOTUBA YA MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA WAKATI WA KUFUNGUA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI UTAKAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA OFISI ZA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI DODOMA**
**TAREHE 19 DISEMBA, 2023**

---

- **Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Mhe. Balozi Prof. Kennedy Godfery Gastorn, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Beatrice Jeremiah Nzobonaliba, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Katibu wa TUGHE Jiji la Dodoma;**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Bi. Zella Kiliat Lwemanyila, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Wageni Waalikwa;**

- **Wanahabari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawashukuru sana kwa heshima kubwa mliyonipatia ya kuwa Mgeni Rasmi na kufungua Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo pia nimepata fursa ya kukutana na Wawakilishi wa Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ninaomba nitumie nafasi hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna ambavyo mmekuwa mkinipatia ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu katika kila Wizara ambayo nimepata kuhudumia. Pamoja na Changamoto mbalimbali zinazowakabili kama taasisi, bado mmeendelea kutekeleza majukumu yenu kwa weledi, uaminifu na ufanisi. Nawasihi mwendelee kuwa na moyo huo wa uzalendo, na katika hili ninawapongeza sana.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Profesa Kennedy Godfrey Gastorn kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sanjari na hilo nawapongeza wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wote waliohusika katika maandalizi ya Mkutano huu muhimu ili kuhakikisha wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanashirikishwa katika ngazi zote za utekelezaji wa shughuli za Ofisi hii kupitia Baraza la Wafanyakazi kwa kushirikiana na Uongozi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kama ulivyotangulia kusema, Mkutano huu umehudhuriwa pia na Makamu Mwenyekiti, Katibu, Wajumbe wa Baraza ambao ni wawakilishi wa wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wageni waalikwa. Nawapongeza kwa kutenga muda wenu na kuja kuhudhuria Mkutano huu siku ya leo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kwa mujibu wa Ibara ya 59(3) & (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote ya kisheria yanayoihusu Jamhuri ya Muungano na amepewa haki ya kuhudhuria na kusikilizwa na Mahakama zote nchini. Sote tunatambua kuwa kazi hii ni nyeti na

inapaswa kufanywa kwa weledi, uaminifu na umakini mkubwa. Kipekee niwapongeze watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri mnayoifanya. Naomba kuwahakikishia kuwa, Serikali inatambua juhudi zenu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Madhumuni ya Baraza la Wafanyakazi, kama wote tunavyoelewa, ni kutoa fursa kwa watumishi, kupitia wawakilishi wao kujadiliana juu ya masuala ya msingi yanayohusu tija na ufanisi kwa upande mmoja na upande mwingine maslahi yao kama watumishi. Nimefurahi kusikia kuwa mikutano ya Baraza la Wafanyakazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hufanyika mara mbili kila mwaka. Hii inaonesha bayana namna ambavyo Menejimenti inatambua umuhimu wa watumishi kushirikishwa katika maamuzi yanayohusu Ofisi yao kupitia Baraza la Wafanyakazi. Nawasihi muendelee na utaratibu huu mzuri kwa faida na maslahi mapana ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taifa kwa ujumla na watumishi wote kwa jumla.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kama ulivyobainisha katika hotuba yako, Mkutano huu umeitishwa kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na taarifa ya hesabu za mwaka 2022/2023. Kama wawakilishi wa Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nawaomba mtumie fursa hii kujadili kwa uhuru na uwazi taarifa hizo ili kupitia Mkutano huu yapatikane

mapendekezo ambayo yataisaidia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali kwa ujumla kutekeleza Mpango na Bajeti yake kwa ufanisi zaidi. Pia, Baraza la Wafanyakazi mahali pa kazi lina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kunakuwepo maelewano, ushirikiano na mshikamano kati ya wafanyakazi na Uongozi wa Taasisi husika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Nimefarijika sana kusikia mafanikio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwemo kuongeza idadi ya watumishi, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki (Government Legal Institutions Integrated Centers-GLIICs) katika mikoa ya Mwanza na Arusha pamoja na Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali jijini Dodoma. Ni wazi vituo Jumuishi hivyo vitakapokamilika vitasaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma za kisheria kwa unafuu na kwa wakati.

Kama Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI ambayo kufikia tarehe 20 Septemba, 2023 ilikuwa na Wanasheria wa Serikali **307**, nawahimiza muendelee kufanya kazi kwa nguvu, juhudi, maarifa na weledi wa hali ya juu na kuunganisha nguvu miongoni mwa wanasheria wote walioko katika sekta ya umma Tanzania ikiwa ni kuunga mkono jitihada za Rais wetu wa Serikali ya awamu ya Sita za kupambana

na vita dhidi ya rushwa, ufisadi na kukosa uzalendo juu ya nchi yetu kwa kuwataka kuijenga Tanzania yenye sifa nzuri na maendeleo hivyo kushamirisha Uchumi wa Kati. Wanasheria 307 walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa ni jeshi kubwa katika sekta ya Sheria kwenye utumishi wa umma. Ninaomba Ofisi yako iweke utaratibu wa namna bora ya kushirikiana nao likiwemo suala zima la mafunzo ili kuwajengea uwezo na kuwaongezea ujuzi, maarifa na kujiamini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Wakati mnajadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mnapaswa pia kujipima na kuangalia namna ambavyo miongozo mbalimbali ya kisera ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inavyozingatiwa. Tunafahamu Taifa letu siyo kisiwa hivyo tunao wajibu wa kushirikiana na mataifa mengine kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kwa kuwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio watekelezaji wa mipango mbalimbali ya Ofisi hususan ile iliyoko katika uga wa sheria ni dhahiri wanapaswa kushirikishwa kwenye maandalizi na utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi wanayoitumikia. Hii ni kwa sababu, hata kama kutakuwa na Sera, Sheria na Kanuni nzuri mahali pa kazi pasipokuwa na ushirikishwaji na ushirikiano baina ya mwajiri na watumishi itakuwa vigumu Taasisi kutimiza malengo yake. Baraza hili lina wajibu wa kuishauri Mamlaka kwa lengo la kuleta tija na mshikamano baina ya

watumishi na mwajiri. Kwa upande wa mwajiri, mtumishi anayetekeleza majukumu yake apatiwe stahili zake na pale anapostahili pongezi apongezwe.  Kupongezwa kwa mtumishi ni motisha na huongeza tija kwa taasisi na kuamsha ari ya kazi kwa mtumishi aliyepongezwa.

Kama kiongozi wa kitaifa ninafahamu zipo changamoto nyingi katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku ikiwemo upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, vyumba ya ofisi pamoja na upungufu wa rasilimali watu na fedha. Changamoto hizi pamoja na nyingine nyingi zilizoainishwa katika hotuba ya Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi ni za msingi sana. Nitumie nafasi hii kuwaahidi kuwa Wizara ninayoiongoza, yaani, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), tutakuwa nanyi bega kwa bega katika kuhakikisha changamoto hizo zinapunguzwa au kuondolewa kabisa kadri bajeti itakavyoruhusu. Katika Mikoa na Halmashauri tutaona namna gani tunaweza  kusaidia kutatua changamoto ya uhaba wa ofisi.

Ningependa kuwahimiza kuwa mwendelee kufanya kazi kwa uadilifu bidiina maarifa, kuheshimu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma wakati Serikali ikiendelea kushughulikia changamoto hizo. Hivyo, msikate  tamaa bali mwendelee kufanya kazi kwa bidii, maarifa, weledi na uzalendo kwa manufaa ya Ofisi yenu na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kutokana na wingi na uzito wa kazi zinatotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mawakili wote **3,359** walio katika Utumishi wa Umma wakiwemo 307 walioko Ofisi ya Rais -TAMISEMI ambao Mwanasheria Mkuu wa Serikali anajukumu la ujumla la kuwasimamia, tutaendelea kushirikiana na Wizara zote husika kujenga hoja ili kadri Uchumi wa Nchi unavyoruhusu, waboreshewe mishahara na maslahi mengine. Hatua hiyo itasaidia kuongeza ari na shauku ya watumishi wa sekta ya sheria katika utumishi wa umma kufanya kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Nimefurahi sana kusikia kuwa kuna Kanuni za Maadili ya Mawakili wa Serikali. Kanuni hizo zitumike kuwadhibiti Mawakili wa Serikali na Maafisa sheria wanaokiuka maadili katika utekelezaji wa majukumu yao – "The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Provision of Legal Opinion by State Attorneys and Law Officers in Public Service) Guidelines, G.N 32/2023 ambazo zinawahusu hata wale wanaofanya kazi katika Wizara na sehemu mbalimbali katika utumishi wa umma zilichapishwa mnamo tarehe 20 Januari, 2023. Natoa rai kwa Mamlaka zote za Ajira

serikalini na kwa Mawakili wote Serikali kuzizingatia na kuzifuata ili kujenga Sekta ya Sheria ya Umma iliyotukuka na yenye heshima machoni mwa jamii.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 8(e) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepewa jukumu la kuwasimamia Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali ambao ni watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Taasisi nyingine za umma. Hivyo, Mawakili wa Serikali wote wanapaswa kuonesha mfano utakaoigwa na watumishi wengine katika Sekta ya Umma.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu ninaomba nitoe wito kwa watumishi wote siyo tu walioko katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali bali pia watumishi wote walioko katika sekta ya sheria kwenye utumishi wa umma. Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria ni ngao muhimu ya Serikali kwa ajili ya kuilinda Serikali lakini pia ni silaha muhimu kwa ajili ya kujilinda dhidi ya maadui wanaoweza kuiendea kinyume Serirkali yetu. Wito wangu kwenu ni kuwataka muimarishe mshikamano mingoni mwenu kwa maslahi mapana ya nchi. Badilishaneni uzoefu, peaneni maarifa na ujuzi ili kuletea heshima miongoni mwenu, taasisi na ofisi za umma mnazozitumikia.

Mawakili wa Serikali walioko Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watumishi

wengine wa sekta ya sheria nje ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wapatiwe mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi hususan katika maeneo yanayohitaji ubobevu ili waweze kuongeza ujuzi na uelewa katika taaluma zao na kuboresha ufanisi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mafunzo kuhusu matumizi ya miongozo iliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuongeza uwezo katika maeneo ya Utungaji wa Sheria, Upekuzi wa Mikataba na Utoaji Huduma za Ushauri wa Kisheria kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yaendelee kutolewa kwa Mawakili wote wa Serikali na Maafisa Sheria wengi zaidi katika taasisi mbalimbali za umma chini ya uratibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza ninaomba kutoa pongezi kwa Uongozi wa Mpito wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (Tanzania Public Bar Association–TPBA). Nawasihi wanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali waendele kutoa ushirikiano kwa viongozi hao na waajiri wa wanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali wawawezeshe ili waweze kushiriki ipasavyo katika Mkutano wa mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali unaotarajiwa kufanyika kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Ni matumaini yangu kuwa majadiliano baina yenu na Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na menejimenti yatatakiwa na hekima, busara, uwazi na maelewano na hapo ndipo mtaweza kutoka na maazimio yenye tija kwa Ofisi na Taifa kwa ujumla. Niwaombe ninyi mliopata bahati ya kuwawakilisha wenzenu muwe wawakilishi wazuri kama wanavyowatajajia. Kuwepo kwenu hapa kumetokana na imani ambayo imejengeka kwa waliowachagua kuja kuwawakilisha, hivyo, thibitisheni imani yenu kwa mnaowawakilisha. Mtakaporudi katika Divisheni na Vitengo vyenu waelezeni kwa kina wenzenu mambo mtakayoafikiana katika mkutano huu ili kujenga uelewa wa pamoja kwa taasisi nzima.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza;**

Naomba kuwashukuru tena na tena kwa kunialika katika Mkutano huu muhimu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni imani yangu kuwa yote yatakayojadiliwa katika Mkutano huu yatasaidia katika kuboresha utendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taifa kwa ujumla na hivyo kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza na Wageni waalikwa, baada ya maelezo hayo, sasa nachukua fursa hii kutamka kwamba Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umefunguliwa rasmi.

**Ninawashukuru sana na kuwatakia siku kuu njema za mwisho wa mwaka.**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**